# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


Simu. 03-3425-4531 FAX. 03-3425-7844
TELEGRAPHIC ADDRESS TANZANREP-TOKYO
Barua pepe: tzrepjp@tanzaniaembassy.or.jp
tokyo@nje.go.tz

UBALOZI WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA
21-9, KAMIYOGA 4-CHOME.
SETAGAYA-KU, TOKYO 158-0098


## TAARIFA

### FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NCHINI JAPAN KWA MWAKA 2027
### *(JAPANESE GOVERNMENT – MEXT SCHOLARSHIP PROGRAM 2027)*

Ubalozi umepokea taarifa ya fursa za ufadhili wa masomo nchini Japan inayotolewa na Serikali ya Japan kupitia Wizara ya Elimu, Utamaduni, Michezo, Sayansi na Teknolojia *(Ministry of Education, Culture, Sports, Science and Technology - MEXT)* kwa mwaka wa masomo 2027. Ufadhili huo ni kwa masomo ya kada mbalimbali kwa ngazi ya:

i) Shahada ya Kwanza *(Undergraduate Studies),*
ii) Umahiri *(Master's Degree),*
iii) Uzamivu *(PhD.)* na
iv) Mafunzo ya Ufundi *(Specialized Training College).*

Taarifa zaidi kuhusu ufadhili ikiwemo, sifa na taratibu za uoambaji zinapatikana kupitia tovuti ya **Ubalozi wa Japan nchini Tanzania** (https://www.tz.emb-japan.go.jp/itpr_en/MEXT2027_00001.html).

Maombi yote kuhusu ufadhili huo, yapitie **Ubalozi wa Japan nchini Tanzania** uliopo Jijini Dar es Salaam, kupitia posta au kuwasilisha ubalozini:

P.O. Box 2577,
Plot No. 1018,
Ali Hassan Mwinyi Rd,
DAR ES SALAAM.

Mwisho wa kutuma maombi hayo ni:

a) tarehe **11 Mei 2026,** kwa *research participants (Masters na PhD);* na
b) tarehe **21 Mei 2026,** kwa *undergraduate/specialized training college.*

Tunashukuru kwa ushirikiano.

**UBALOZI WA TANZANIA NCHINI JAPAN**
**TOKYO**
**24 Aprili 2026**